035713655

KENYA NATIONAL PREDICTION TESTS

516004

# KCPE

# KISWAHILI
## SEHEMU YA KWANZA
## LUGHA

**Muda: Saa 1 dakika 40**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

**SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI.**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**
5. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
6. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
7. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
8. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
9. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

   **Mfano:**

   **Katika kijitabu cha maswali:**

   **22.** Barua ya kuomba kazi huitwa
   - A. waraka
   - B. barua maalum
   - C. barua ya kiofisi
   - D. Barua rasmi

   Jibu sahihi ni **D**

   **Katika karatasi ya majibu:**

   2. [A] [B] [C] [D] 12. [A] [B] [C] [D] 22. [A] [B] [C] [D] 32. [A] [B] [C] [D] 42. [A] [B] [C] [D]

   Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **22**, kisanduku chenye herufi **D** ndicho kilichochorwa kistari.
10. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
11. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**

906504

© Mtihani Bora

GEUZA UKURASA

***Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 hadi 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne.***


***Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Gari ____1____ ____2____ lilipofika ____3____ ____4____ ____5____ miongoni mwetu tulijisaili ni ____6____ shangingi ____7____ kama ____8____ lingaliweza kufika ____9____ walalahoi. ____10____ kutaamali____11____ ndipo____12____ kwamba____13____ ____14____ kuomba____15____ ulikuwa tayari.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. kubwa | B. likubwa | C.mkubwa | D.jikubwa |
| **2.** | A.hili | B.lile | C.hilo | D.yale |
| **3.** | A.huku | B.hapa | C.pale | D.humu |
| **4.** | A.kwangu | B.kwake | C.kwetu | D.mwetu |
| **5.** | A.wingi | B.sote | C.wengine | D.wengi |
| **6.** | A.mbona | B.aje | C.vipi | D.lini |
| **7.** | A.ghali | B.rafi | C.ghafi | D.muflisi |
| **8.** | A.lele lile | B.lili hili | C.iyo hiyo | D.ile ile |
| **9.** | A.kunakoliwa | B.kunakoketi | C.kunakoliliwa | D.kunakokaa |
| **10.** | A.kisha ya | B.licha ya | C.mbali na | D.halafu ya |
| **11.** | A.mzimu | B.msimu | C.risimu | D.isimu |
| **12.** | A.tulipotaamali | B.tuluipojua | C.tulipoaka | D.tulipomaizi |
| **13.** | A.arubaini | B.kaski | C.hafla | D.hamsini |
| **14.** | A.za | B.na | C.kwa | D.ya |
| **15.** | A.kula | B. uchaguzi | C.kura | D.ujumbe |

***Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi.***

16. Wakati wa jua kuzama huitwaje?
    A. Mawio
    B. Macheo
    C. Machweo
    D. Kuchwa
17. Jakaiti alimlilia mtoto si sawa na kusema:
    A. Alitaka mtoto
    B. Alilia mtoto
    C. Alilia kwa niaba ya mtoto
    D. Alishtaki kwa mtoto
18. Tegua kitendawili hiki:
    **Canga'aa, chapendeza lakini hakifikiwi**
    A. jua B. mbingu
    C. ngazi D. kivuli
19. ***Andika wingi wa***
    **Wembe mpya ulikatiwa ukucha wa mtoto**
    A. Mawembe mpya zilikatiwa kucha za watoto
    B. Nyembe zipya zilikatiwa makucha za mtoto
    C. Wembe mpya zilikatiwa makucha za watoto
    D. Nyembe mpya zilikatiwa kucha za watoto
20. ***Tambua aina ya neno lililopigiwa mstari:***
    ***Mtoto alisimama kando ya barabara.***
    A. Kihisishi B. Kielezi
    C. Kihusishi D. Kivumishi
21. Ili kupima usawa wa ukuta, mwashi hutumia
    A. parafujo B. timazi
    C. keekee D. bisibisi
22. Vitu viwili ni jozi na miaka kumi ni
    A. mwongo B. karne
    C. milenia D. korija
23. Ni kundi lililo na sauti sighuna pekee?
    A. /d/, /v/, /z/, /b/
    B. /ch/ , /t/, /p/, /s/
    C. /a/, /e/, /i/, /o/, /u/
    D. /dh/, /y/, /sh/, /th/
24. Ikiwa jana ilikuwa Jumapili tarehe tano, kitojo itakuwa lini?
    A. Ijumaa tarehe ashara
    B. Jumanne tarehe saba
    C. Jumamosi tarehe edashara
    D. Jumapili tarehe edashara
25. Tambua umbo hili

    A. Msalaba B. Nyota
    C. Kopa D. Hilali
26. Akisami hii $^2/_3$ huitwaje
    A. Thuluthi mbili B. Nusu tatu
    C. Tusui mbili D. Subui mbili
27. Mfalme ni kwa kasri kama vile nyuki ni kwa
    A. jana B. shibli
    C. zizi D. kizimba
28. Sentensi ambayo imetumia **-na-** ya kumiliki ni
    A. Atieno ana huzuni
    B. Kiko na digali
    C. Omar ana mpira
    D. Watoto waipigana
29. Nomino kivinimbi iko katika ngeli gani?
    A. KI - VI B. A - WA
    C. I - ZI D. LI - YA
30. **800,396**
    A. Laki nane, mia tatu elfu tisini sita
    B. Laki mia nane, elfu tatu tisini na sita
    C. Laki themanini, mia tatu tisini na sita
    D. Laki nane, mia tatu tisini na sita

***Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali kutoka 31 - 40.***

Matatu matata! kutoka mjini hadi mtaani ni mapeni matatu. Labda ndiyo asili ya neno matatu. Waswahili husema kuwa mgala muue na haki yake umpe. Ukweli wa mambo ni kuwa matatu ni kiungo muhimu cha jamii. Matatu zimesaidia sana kurahisisha usafiri Afrika mashariki na kati. Magari haya yana umaarufu kwa mambo matatu.

Kwanza, bei ya usafiri ni nafuu kwa vile wakati mwingine hupanda na nyakati zingine ikashuka. Aidha, mtu anapokuwa amepungukiwa na uzito mfukoni, huweza kuzungumza na utingo na akasafiri bila ya wahaka wala rangaito.

Pili, matatu zina umaarufu wa ukaidi ambao ni abiria wanaofaidi. Matatu huweza kusimama popote na kuchukua ama kushusha abiria, jambo ambalo humpunguzia abiria udhia wa kukimbilia kituoni pa mabasi yasiyokuwa na tabia za kusimama popote.

Tatu na hatari, ni desturi ya matatu kutojaa kwa hivyo popote inapoegeshwa, nafasi haikosi kwa abiria pamoja na kwamba magari haya huweza kujipenyeza kando ya njia na kufika yaendako kwa haraka na hivyo huokoa muda wa wasafiri. Hata hivyo, matatu zina madhara kadhaa. Matatu zimelaumiwa kwa kusababisha ajali nyingi za barabarani pamoja na vifo vya watu wengi. Magari haya pia yanaudhi abiria wasiopenda muziki wa sauti ya juu sana ambao ni hatari kwa masikio.

Wanapohisi kudhulumiwa, madereva na utingo hufanya migomo ambayo huishia kuwa tesa wateja wao mbali na visa vya uhalifu wanavyoshiriki wakiwa migomoni. Ingawa ni sekta muhimu kwa jinsi inavyochangia uchumi wa taifa kwa kutoa nafasi nyingi za ajira, sera maalum zinastahili kuundwa na kutekelezwa ili kudhibiti ukaidi wake.

---

**31.** Mbona mwandishi anaanza kwa kauli kuwa matatu matata?

A. Anachoshwa na kuwapo kwa matatu
B. Anaonyesha kuudhika na matatu
C. Matatu husababisha balaa nyingi
D. Kuonyesha kuwa matatu zinazua utata

**32.** Mapeni matatu yaliyotozwa kwa waendao mjini ilikuwa ndiyo

A. machorombozi
B. kiokozi
C. koto
D. nauli

**33.** Katika aya ya **kwanza,** mwandishi anasema kuwa

A. matatu zinasaidia sana katika usafiri
B. matatu zinaleta hasara sana katika miji
C. nguo japo ni pambo la mwili zitumiwe kwa uangalifu ili tudumishe maadili
D. nguo zitumiwe zilizo za bei ghali ili kuonyesha uwezo wetu

**34.** Mwandishi anasema kuwa bei ya kusafiria katika matatu

A. ni ya kufyatuka kwa manufaa ya wenye magari
B. ni tahafifu na haina wa kuidhibiti
C. ni nafuu na wakati mwingine hupanda na kushuka
D. Ni ghali na katu hazishuki hata mara moja

**35.** Vita vya panzi furaha ya kunguru. Ni kunguru yupi anayefaidi kwa mujibu wa kifungu?

A. Abiria kutokana na makuruhu ya matatu
B. Matatu kutokana na wepesi wa abiria
C. Abiria kutokana na uzuri wa barabara zetu
D. Matatu kutokana na udhibiti wa nauli.

**36.** Matatu hurahisisha mambo kwa abiria kwa sababu?

A. Hutoza nauli ghali na kuvunja sheria za barabarani
B. Huwachukua na kuwashusha abiria popote
C. Huchukua abiria popote na kuvunja sheria za nchi
D. Huwashusha abiria popote na kuwatoza nauli yoyote

**37.** Matatu huamini kuwa haiwezi kujaa wala kukosa nafasi na kwa hivyo.

A. Huweza kutanua gari ili kuwa na nafasi kubwa zaidi
B. Huishia kubeba abiria kupita kiasi kinachohitajika
C. Huweza kubeba abiria waliokosa nafasi katika mabasi
D. Huweza kuwaokoa abiria waliochelewa

**38.** Matatu yameshutumiwa kwa madhara hasa.

A. kuimarisha msongamano wa magari
B. kukomesha msongomano wa magari barabarani
C. kuepuka msongamano wa magari njiani
D. kusababisha vifo kwa ajali za barabarani

**39.** Madereva na utingo wanapohisi kudhulumiwa

A. huzuia abiria kufika kazini kwa wakati
B. hasira zao huishia katika migomo inayowatesa abiria
C. huwagomea abiria na kuwatesa waendapo kazini
D. huzuia waajiri kuwafuta abiria wanaochelewa kazini

**40.** Kifungu kinaangazia manufaa ya matatu licha ya kuwa na upungufu wake. Ama kweli

A. mbio za sakafuni huishia ukingoni
B. hakuna masika yasiyo na mbu
C. mgala muue na haki umpe
D. hakuna marefu bila kikomo

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali ya 41 - 50.***

Visa vya utovu wa usalama vimekithiri kiasi cha kuwatia raia roho mkononi. Kila wakati wa matangazo ya habari redioni, runinga na hata magazetini, hapakosi habari za wawili au watatu kushambuliwa na kuuawa kwa risasi na majambazi.

Wauaji hawa wamezidi kiburi na ujasiri kwani hata vituo vya polisi sasa havina uhakika wa usalama kwa kuwa navyo pia hushambuliwa na magaidi wa mhanga. Haijulikani hasa sababu kuu ya majambazi kuamua kuwaua maafisa fulani wa polisi na wanajeshi.

Hata katika maabadi, hali imekuwa ya wasiwasi kwa mintarafu ya milipuko na mashambulizi yaliyoshuhudiwa siku za hivi karibuni. Wanaokwenda maabadani hawajui na kujumuika katika ibada. Tumeshuhudia viongozi wa kidini wakiomba serikali kuwapa ruhusu ya kubeba silaha wakiwa kwenye ibada. Je inawezekana kuwa hata masalahina hawaamini ikiwa Mungu anaweza kuwalinda?

Cha msingi ni kwamba, serikali za magatuzi na serikali kuu lazima kukaa mezani na kubuni mikakati madhubuti ya kudhibiti usalama ili uzalishaji kuimarika. Tuelewe kuwa usipoziba ufa utajenga ukuta.

---

**41.** Neno **'vimekithiri'** lilivyotumika katika habari lina maana ya
A. kuanza B. kukoma
C. kupungua D. kuzidi

**42.** Kwa mujibu wa sentensi ya kwanza,
A. watu wana ukweli kuhusu usalama wao
B. watu wana wasiwasi kuhusu usalama wao
C. watu wana uhakika na usalama wao
D. watu wanaishi na roho zao viganjani

**43.** Katika aya ya kwanza, mwandishi anasema kuwa
A. kila wasaa kuna taarifa za waliofariki mikononi mwa majambazi
B. Vyombo vya habari vinaeneza habari za wanaowaua wananchi
C. wanaouawa hawakosi kushirikiana na vyombo vya majambazi
D. Wanaowaua majambazi ni vyombo vya habari

**44.** Kiburi cha wauaji hawa kinadhihirika mno kwa kuwa sasa
A. licha ya kuwashambulia waja, hata vituo vya polisi hawajaviacha
B. Pamoja na vyombo vya habari, pia wanashirikiana na polisi
C. Pasipo vituo vya polisi, wameshindwa kupenya kwenye kambi
D. Kinyume na vituo vya polisi, hata vyombo vya habari vinashambuliwa

**45.** Kwa mujibu wa kifungu, vituo vya polisi hushambuliwa na
A. wauaji wa kujitolea
B. wakaidi wenye mhanga
C. wauaji wa kujitoa
D. wauaji walio hanga

**46.** Katika aya ya **pili,** mwandishi ana maoni kuwa
A. vyombo vya habari vina mashtaka mengi ya kujibu
B. vyombo vya habari vinawaficha majambazi fulani
C. Majambazi wamewaua polisi fulani
D. Majambazi wana njama ya kuwaua askari fulani

**47.** Siku za hivi karibuni kumeshuhudiwa visa vya:
A. uchochezi makanisani
B. mashambulizi maabadani
C. vyombo vya habari vinavyowatetea majambazi
D. Wananchi wakiwa na utulivu

**48.** Mikasa ya mashambulizi maabadani imesababisha haya ila
A. idadi ya waumini kuongezeka maradufu
B. viongozi wa kidini kutaka bunduki za kujilinda
C. Masalihina kuwa na wahaka kuhusu wenzao maabadini
D. Ugomvi baina ya wanaoamini na wasioamini

**49.** Mwandishi anahitimisha kwa kauli kuwa:
A. vyombo vya habari visikome kushirikiana na majambazi
B. kuwapo kwa usalama madhubuti kunaweza kuimarisha uchumi
C. Uksoefu wa usalama unaweza kuimarisha usalama
D. Msingi wa usalama ni vyombo vya habari

**50.** Kichwa kinachofaa habari hii ni
A. serikali kuu
B. maabadi
C. polisi na wanajeshi
D. usalama

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako**

***Malizia insha yako kwa maneno haya:***

……………………………………….*nilitanabahi kuwa dawa za kulevya huleta hasara nyingi mno.*